

## **TAARIFA KWA UMMA**

### **MIKATABA YA UNUNUZI WA UMEME NA BEI YA UMEME TOKA KWA WAZALISHAJI WADOGO WADOGO**

Serikali ya Jamhuri ya Tanzania kupitia Wizara ya Nishati na Madini na kwa msaada wa Benki ya Dunia inapenda kuharakisha huduma ya umeme iwafikie watanzania wengi zaidi. Kwa kutekeleza mradi wa Nishati Tanzania (TEDAP), serikali inaendeleza miradi ya umeme rejea (renewable energy) hapa nchini kwa kuwavutia wawekezaji binafsi ili washiriki katika maendeleo ya miradi ya umeme midogomidogo.

Ili kufanikisha lengo hili, Wizara ya Nishati na Madini, baada ya kuwahusisha wadau mbalimbali, ilitayarisha Mkataba wa Ununuzi wa Umeme (Standardised Power Purchase Agreement) na Mkataba wa Bei ya Kununua Umeme (Standardised Power Purchase Tariff) zitakazotumika kuunganisha na kuuza umeme katika gridi kuu na gridi ndogo. Mikataba hiyo iliidhinishwa na Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kwa mujibu kifungu namba 17 cha Sheria, Sura ya 414 (EWURA Act, Cap 414). Utaratibu wa kukokotoa bei ya umeme unaweza kufanyiwa marekebisho kila baada ya miaka mitano baada ya kuidhinishwa isipokuwa kama kuna jambo la msingi. Bei ya umeme kwa miradi midogo midogo inarekebishwa kila mwaka kulingana na mabadiliko ya gharama za uendeshaji zilizo nje ya uwezo wa mwekezaji. Bei hiyo hurekebishwa na Kikosi Kazi cha Maendeleo ya Miradi Midogo Midogo (Working Group on Small Power Development (WGSPD) ambacho kinawezeshwa na EWURA.

Wawakilishi wa WGSPD wanatoka Wizara ya Nishati na Madini, Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam, Baraza la Ushauri la Watumiaji Huduma zinazodhibitiwa na EWURA, "Tanzania Private Sector Foundation", Rural Energy Agency, TANESCO na EWURA kama mtazamaji "observer" ambao hukutana kila mwaka, na kwa kutumia taarifa zilizowasilishwa hukokotoa bei ya umeme kwa miradi midogo midogo na kuwasilisha EWURA ili iidhinishwe.

- i. Bei iliyopendekezwa katika mwaka 2010 ya kununua umeme toka kwa Wazalishaji Umeme Wadogo wadogo ambao huunganishwa katika gridi kuu ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 1 hapa chini:

**Jedwali Na. 1: Bei ya Umeme kwa Wazalishaji wadogo wadogo – Gridi kuu**

Wastani wa bei ya Umeme kwa Wazalishaji Wadogo wadogo		110.30	TZS/kWh
Bei itabadilika kulingana na msimu	Msimu wa jua/kiangazi	Agosti - Novemba	132.36
	Msimu wa mvua/masikana	Januari - Julai na Desemba	99.27

- ii. Bei iliyopendekezwa katika mwaka 2010 ya kununua umeme toka kwa Wazalishaji Umeme Wadogo wadogo ambao huunganishwa katika gridi ndogo ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 2 hapa chini:

**Jedwali Na. 2: Bei ya Umeme kwa Wazalishaji Wadogo wadogo – Gridi ndogo**

Wastani wa bei ya Umeme kwa Wazalishaji Wadogo wadogo	<b>368.89</b>	TZS/kWh
-------------------------------------------------------	---------------	---------

Kulingana na kifungu namba 19 (2) (b) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Sura ya 414 (EWURA Act, Cap 414), wadau wote wanakaribishwa kuwasilisha maoni yao, kwa barua au vinginenvyo, juu ya uhalali wa Bei ya Ununuzi wa Umeme toka kwa Wazalishaji Umeme Wadogo wadogo katika kipindi cha wiki tatu (siku 21) tokea tarehe ya tangazo hili.

Taarifa zaidi zinapatikana kwa kuiandikia EWURA kwa anuani iliyotajwa hapo juu:-

**Limetolewa na;**

**Mkurugenzi Mkuu, EWURA**